**UMOJA WA WAZAZI TANZANIA**
**(JUMUIYA YA CCM)**
**SHULE YA SEKONDARI KIBO**

**Simu:0773777 015**
**0757 656 994**
**Barua pepe:** kibosecondary@gmail.com
**Tovuti:** www.kibosecondary.sc.tz

**Barua zote zitumwe kwa**
**Mkuu wa Shule,**
**S.L.P 836,**
**MOSHI-TANZANIA**
**Tarehe: 28/10/2024**

Ndugu Mzazi/Mlezi

## YAH: KUJIUNGA NA MASOMO YA AWALI YA KIDATO CHA TANO (PRE- FORM FIVE).

## 1.0 UTANGULIZI

St. Thomas Aquinas Foundation ambaye ni mwekezaji katika **shule ya sekondari Kibo** na shule ya **sekondari Wari** ameandaa programu maalumu ya Masomo ya Awali ya Kidato cha Tano (**Pre-Form Five**) itakayofanyika kuanzia **tarehe 15 Januari, 2025** shuleni Kibo sekondari. Programu hii ni muhimu kwa wanafunzi waliomaliza Kidato cha Nne ili kuwaandaa vema kujiunga na Kidato cha Tano katika tahasusi wanazotarajia kuzisoma.

Dhamira ya mafunzo haya ya awali ni kumwandaa mwanafunzi kujiunga na kidato cha tano kwa tahasusi anayotarajia kuifanya. Wakati wa mafunzo haya ya awali ni muda pekee ambao mwanafunzi anaweza kujifanyia tathmini juu ya uwezo wake katika kukabiliana na masomo ya tahasusi anayoitarajia kuifanya.

Mafunzo ya awali yatamsaidia mwanafunzi kuwa na uzoefu na tahasusi, hivyo kufanya maamuzi sahihi wakati wa kujiunga na kidato cha tano. Wanafunzi wengi wamekuwa na changamoto za machaguo ya tahasusi kutokana na kutokuzifahamu kwa undani. Hali hii inawafanya kutumia muda mrefu hadi kuzizoea na kuanza kusoma kulingana na nguvu inayotakiwa kuwekezwa katika tahasusi husika. Ikiwa mwanafunzi atashindwa kuhimili uzito wa tahasusi humlazimu kuibadili wakati muda umekwenda sana au kusoma tahasusi asiyokuwa na uwezo nayo.

Wakati wa maandalizi haya ni muhimu sana, hivyo uongozi wa shule kwa kuitambua changamoto hiyo umeandaa programu hii kama sehemu ya kufanya uelekezi katika tahasusi ambazo mwanafunzi anatarajia kufanya atakapojiunga na kidato cha tano.

Sambamba na dhamira tajwa hapo juu, programu hii inalenga hasa kumpatia mwanafunzi mbinu bora za kujisomea ili aweze kupata matokeo makubwa kama ilivyo desturi katika shule yetu.
Lakini pia ni program muhimu kwani itampatia mwanafunzi muda wa kutosha katika kujisomea masomo yake pamoja na kuandaliwa mapema jambo litakalompatia kujiamini na hatimaye kumfanya kuwa mahiri katika tahasusi atakayokuwa ameichagua.

## 2.0 MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya Sekondari Kibo ipo Mkoa wa Kilimanjaro, Manispaa ya Moshi, kata ya Longuo B. Umbali wa kilometa sita (6) kutoka kituo kikuu cha mabasi Moshi au kilometa tano (5) kutoka Keep Left ya Arusha.

## 3.0 JINSI YA KUFIKA SHULENI

- Kwa unayetumia usafiri wa umma kutoka Moshi Mjini utapanda bajaji itakayo kuleta moja kwa moja shule ya sekondari Kibo.
- Aidha, kwa unayetumia usafiri binafsi kutoka Moshi mjini utalazimika kuja hadi Keep Left ya Arusha na kufuata barabara ya kuelekea KIBOSHO KIRIMA. Kwa kufuata barabara hiyo, shule iko mita chache mbele ya International School of Moshi (ISM).

## 4.0 TAHASUSI ZITAKAZOFUNDISHWA

Wanafunzi wa mafunzo ya awali ya kidato cha Tano kulingana na machaguo yao, watafundishwa masomo yafuatayo: -

| NA. | TAHASUSI | MASOMO KATIKA TAHASUSI |
|---|---|---|
| 1. | PCB | PHYSICS, CHEMISTRY, BIOLOGY |
| 2. | PCM | PHYSICS, CHEMISTRY, ADVANCED MATHEMATICS |
| 3. | PGM | PHYSICS, GEOGRAPHY, ADVANCED MATHEMATICS |
| 4. | EGM | ECONOMICS, GEOGRAPHY, ADVANCED MATHEMATICS |
| 5. | CBG | CHEMISTRY, BIOLOGY, GEOGRAPHY |
| 6. | HGE | HISTORY, GEOGRAPHY, ECONOMICS |

**NB:** Wanafunzi watakao soma tahasusi za PCB, CBG na HGE watafundishwa pamoja na somo la BASIC APPLIED MATHEMATICS.

## 5.0 GHARAMA

Gharama ya jumla kwa programu hii ni shilingi **Laki Nane** (Tsh. 800,000), Ikiwa ni gharama jumuishi ya vitu vifuatavyo: -

1. Gharama za ufundishaji (Tution fee).
2. Chakula na malazi (Meals and Accommodation).
3. Sare ya shule(uniform).
    - T-shirt mbili (2)
    - Sweta mbili (2)
    - Suruali mbili (2) kwa wavulana.
    - Sketi mbili (2) kwa wasichana.
4. Mashuka mawili (2).
5. Huduma ya kwanza (First Aid). Wanafunzi wenye bima za afya wanapaswa kuja nazo ili kuwasaidia wanapohitaji matibabu zaidi kutoka katika hospitali wanazopelekwa kwa matibabu.

## 6.0 MAHITAJI ANAYOPASWA KUJANAYO MWANAFUNZI

| Na. | Vifaa |
|---|---|
| 1 | Daftari (3 Quire Counter book) tano (5), kalamu, penseli na rula |
| 2 | Scientific calculator (*fx*-991ES PLUS) |
| 3 | Godoro lenye ukubwa wa inchi 2.5 |
| 4 | Chandarua ya pembe nne. |
| 5 | Mto na foronya. |
| 6 | blanketi |
| 7 | Sabuni ya kufulia na kuogea. |
| 8 | Taulo |
| 9 | Mswaki, dawa ya meno na mafuta ya kujipaka. |
| 10 | Sahani, kijiko na kikombe. |
| 11 | Ndoo mbili (2), kubwa moja na ndogo moja. |
| 12 | Mashati mawili (2) meupe yenye mikono mifupi. |
| 13 | Nguo za ndani za kutosha (underwear). |
| 14 | Soksi jozi tatu (3), wavulana soksi nyeusi na wasichana soksi nyeupe. |
| 17 | Tracksuit (dark blue) yenye mstari mweupe. |
| 18 | Viatu vyeusi vyenye Kamba. |
| 19 | Pull-neck mbili (2), nyeusi au damu ya mzee (Maroon Colour) |

## 7.0 MWONGOZO WA MALIPO

Malipo ya kozi ya awali ya kidato cha Tano yafanyike kupitia akaunti namba zifuatazo:-

a. **Malipo ya Ada**
   - Cooperative Rural Development Bank (CRDB)
     Jina la Akaunti – **ST. THOMAS AQUINAS FOUNDATION**
     Namba ya Akaunti-**0150626495400**

b. **Pesa ya Matumizi ya mwanafunzi (Pocket Money)**
   - Cooperative Rural Development Bank (CRDB)
     Jina la Akaunti – **ST. THOMAS AQUINAS FOUNDATION**
     Namba ya Akaunti-**015C626495401**

Muda wa mwanafunzi kuripoti shuleni ni kuanzia saa **saa 2:00 Asubuhi** hadi **saa 10:00 jioni** ya tarehe atakayoripoti shule, akiwa na stakabadhi ya malipo (pay-in-slip) tayari kwa kuanza masomo.

**ANGALIZO: MALIPO YOTE YAFANYIKE BANK**

**Wako katika ujenzi wa Taifa**

**…………………………..…….**
**ANDREW SHIJA LIKALILO**
**MKUU WA SHULE**